



# Sauti za Walimu na Wanafunzi:

## Muhtasari wa utafiti wa KiuFunza:

### Kuhusu KiuFunza

KiuFunza – ni kifupi cha maneno ya Kiswahili Kiu ya Kujifunza - ni programu ya malipo kwa walimu kutokana na utendaji kazi wao. Ni mfumo wa motisha unaounganisha malipo ya bakshishi kwa walimu na viwango vya ujuzi wa wanafunzi wao katika kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK). KiuFunza ilianza kutekelezwa na kufanyiwa majaribio shuleni kote nchini Tanzania tangu mwaka 2013. Mfumo wa KiuFunza unawalenga walimu wa madarasa ya 1-3, kwasababu walimu hawa wanawajibika kufundisha stadi muhimu za KKK na wafundisha madarasa yenye wanafunzi wengi zaidi. Tathmini huru za programu hii ya KiuFunza zinaonesha kwamba bakshishi inayotolewa kwa walimu inaleta ongezeko kubwa kwenye viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa takriban theluthi moja ya kile wanachojifunza katika mwaka mmoja wa masomo.

### Maelezo kuhusu takwimu

Matokeo yote kwenye muhtasari huu wa KiuFunza yametokana na utafiti wa awali na uchambuzi wake uliofanywa nchini Tanzania mwaka 2019 na taasisi ya RISE Tanzania. RISE Tanzania ni sehemu ya jitihada ya RISE (Utafiti wa Kuboresha Mifumo ya Elimu), ambao ni program ya kimataifa ya utafiti yenye makao yake makuu katika Chuo Kikuu cha Oxford[1]. Utafiti wa msingi wa RISE ulifanyika kati ya tarehe 18 Februari na 10 Mei, 2019. Uliandaliwa na kutekelezwa na Timu ya Utafiti ya RISE Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya utafiti yenye makao yake makuu mjini Bukoba, iitwayo Economic Development Initiatives (EDI). Ukusanyaji wa takwimu ulifanyika kwenye shule za msingi zipatazo 397, Maafisa Elimu Wilaya 22, na maafisa Elimu Kata wapatao 397 kutoka mikoa sita ya Tanzania: Simiyu, Pwani, Singida, Tanga, Songwe na Kigoma, walishiriki.

1 Uandikishaji wa Watoto shuleni umeongezeka kwa kasi duniani kote, lakini mamilioni ya watoto hutumia miaka mingi shuleni bila kupata ujuzi wa msingi katika KKK. Utafiti wa Kuboresha Mifumo ya Elimu (RISE) ni mpango wa kimataifa wa utafiti unaochunguza jinsi mifumo ya elimu inavyoweza kuondokana na janga hili.

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.


S. L. P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
S: +255 22 266 4301 | B: info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti

Utafiti wa awali uliandaliwa ili kutoa taarifa za kina na zenye uwakilishi wa kitaifa kuhusu hali ya elimu ya msingi nchini Tanzania.

## Wanafunzi

**Jambo la 1: Wanafunzi wengi wanataka kuhitimu elimu ya sekondari au zaidi ya hiyo**
Wanafunzi wa shule za msingi wa Darasa la 2 na 3 waliulizwa: *Fikiria huna vikwazo na unaweza kuendelea na masomo kwa muda mrefu kadri unavyopenda. Je, ungependa ufike kiwango gani cha elimu rasmi?*

**Kielelezo cha 1: Kiwango gani cha elimu rasmi ungependa kuhitimu?**




**Chanzo:** Utafiti wa awali wa RISE, 2019


Wanafunzi wachache (karibu asilimia 20) wanaridhika na kuhitimu elimu ya msingi pekee. Takriban asilimia 40 ya wasichana na wavulana wangependa kuhitimu elimu ya sekondari, na karibu mwanafunzi mmoja kati ya watatu angependa kumaliza chuo kikuu. Kwa upande wa uandikishaji, ambapo uandikishaji wa jumla wa wanafunzi wa sekondari nchini Tanzania ulikuwa asilimia 31.4% mwaka 2020, Tanzania inapiga hatua kwa wanafunzi wengi kupenda kuendelea na masomo ya sekondari. Lakini idadi ya wanafunzi waliodahiliwa vyuo vya elimu ya juu ilikuwa asilimia 7.8 tu mwaka 2020[2]

Twaweza inawapa motisha walimu wa shule za msingi ili wafanye bidii kuboresha stadi za msingi (kusoma, kuhesabu, kuandika), ili wanafunzi wasimalize shule bila kujua kusoma hadithi, kuzidisha au kuandika. Dira yetu inatuelekeza kuiona shule ya msingi kama mahali ambapo hukuza vipaji vya wanafunzi wote, na siyo mahali pa kuchuja wanafunzi kwa kuchukua wanaofanya vizuri tu darasani. Walimu makini wanaweza kuboresha nafasi za wanafunzi kutimiza malengo yao ya elimu.

2 Takwimu za uandikishaji kutoka Taasisi ya Takwimu ya UNESCO (kupitia data.worldbank.org, takwimu zilichukuliwa Februari 2022). Uwiano wa uandikishaji wa jumla ni uwiano wa jumla wa uandikishaji, bila kujali umri, kwa Watoto wenye umri uliopangwa rasmi kujiunga na shule kwenye ngazi ya elimu iliyotajwa.

### Jambo la 2: Wanafunzi wengi wanataka kuwa walimu!

**Kielelezo cha 2: Ni kazi gani unapenda kufanya ukiwa mkubwa?**




**Chanzo:** Utafiti wa awali wa RISE, 2019. Kutokana na mahojiano na Wanafunzi wa darasa la II-III. Kazi zilizotajwa kwa 1% au Zaidi ndizo zimejumuishwa kwenye ripoti.

Wanafunzi waliulizwa ni aina gani ya kazi wangependa kufanya watakapokuwa wakubwa. Walimu wanaonekana ni mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wengi. Wanafunzi wengi zaidi wanapenda kuwa walimu, huku asilimia 41 ya wasichana walisema wanataka kuwa walimu na wavulana asilimia 33 wanapenda kufanya kazi hiyo. Kazi nyingine zinazofuatia kupendwa na wanafunzi mbali na ualimu ni Ukulima na Udaktari, ikifuatiwa na udereva kwa wavulana.


## Motisha kwa Waalimu

### Jambo la 3: Walimu wengi wanapenda zaidi kazi ya ualimu kuliko nyingine

Walimu waliulizwa: *Kama ungeweza kuanza upya, ungechagua ualimu kama ajira yako?* Majibu yao yalikuwa mazuri. Walimu wengi (asilimia 75) walisema wangechagua tena kazi ya kufundisha. Wakati huo huo, baadhi yao (asilimia 25) walisema wangependa kazi tofauti na ualimu.

Matokeo mengine ya utafiti (hayajaoneshwa kwenye mchoro) yanaonesha kuwa vipengele vya kazi ambavyo walimu hawaridhishwi navyo ni mishahara midogo (asilimia 48 hawaridhiki) na fursa adimu za kupandishwa vyeo (asilimia 44 hawaridhiki).

**Kielelezo cha 3:** ***Kama ungeweza kuanza upya, ungechagua ualimu kama ajira yako?***




**Chanzo:** Utafiti wa Awali wa RISE, 2019.


*Maelezo kuhusu sampuli ya walimu: sampuli ya RISE ilitumia karibu walimu 8 kwa kila shule (au 70% ya walimu wote wa shule zilizochaguliwa). Walimu wote wa darasa la 2 na 3 walichaguliwa; sampuli iliyobaki ilichaguliwa kinasibu kutoka madarasa ya 1, 4 na 7*

## Jambo la 4: Walimu wengi hawapendelei kufundisha madarasa ya mwanzo

Walimu wa shule za msingi waliulizwa ni daraja gani wangependa kufundisha kama wangepewa uhuru wa kuchagua. Kwenye uchambuzi wetu tuliweka makundi ya madarasa ya aina mbili; madarasa ya juu (kama mwalimu alitaja kati ya darasa la 4-7) na madarasa ya mwanzo (Darasa la 1-3).

Kielelezo cha 4 kinaonesha madarasa wanayopenda kufundisha walimu kwa sasa, *madarasa ya mwanzo* ni kama mwalimu anafundisha darasa la 1-3 tu; *madarasa ya juu* ni kama mwalimu anafundisha darasa la 4-7; na *madarasa yote* kama mwalimu amepangiwa darasa la juu na la mwanzo. Jumla inaonesha upendeleo wa walimu wote (bila kujali darasa analofundisha sasa).

**Kielelezo cha 4: Upendeleo wa walimu wa madarasa ya kufundisha**




**Chanzo:** Utafiti wa awali wa RISE, 2019.

Matokeo yanaonesha kuwa walimu wengi wa shule za msingi hupendelea kufundisha madarasa ya juu (Darasa la 4-7). Ni asilimia 17 tu ya walimu wote walionesha kupendelea kufundisha madarasa ya mwanzo. Miongoni mwa walimu ambao kwa sasa wanafundisha madarasa ya juu pekee, wengi wao asilimia 96 wanapendelea kubaki kufundisha madarasa hayo. Lakini upendeleo wa kufundisha madarasa ya juu pia unaoneshwa na walimu ambao kwa sasa wanafundisha madarasa ya mwanzo: asilimia 63 ya walimu wanaofundisha madarasa ya mwanzo kwa sasa wangependelea kuhamia kufundisha madarasa ya juu.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha walimu kutovutiwa kufundisha watoto wa madarasa ya mwanzo katika shule za msingi. Hii ni changamoto kwa nchi kwa sababu ujuzi wa KKK ambao ni msingi muhimu wa kusoma, kuandika na kuhesabu hufundishwa katika madarasa ya mwanzo ya shule za msingi.


## Jambo la 5: Walimu wa madarasa ya mwanzo wana makadirio makubwa ya uwezo wa wanafunzi wao kuliko uhalisia

Katika utafiti wa awali wa RISE, walimu wa darasa la 1, 2 na 3 waliulizwa "*Ni wanafunzi wangapi kwenye darasa lako ambao wanaweza kusoma hadithi fupi ya Kiswahili ya ngazi ya darasa la 2 (hadithi fupi ya sentensi tano); na kujibu maswali ya uelewa*?". Walimu walikadiria kuwa 70% ya wanafunzi wao wangeweza kusoma na kuelewa.

Swali kama hilo liliulizwa kwa hesabu za kujumlisha za kiwango cha darasa la 2: "Ni wanafunzi wangapi kwenye darasa lako ambao wanaweza kufanya hesabu za kujumlisha za ngazi ya darasa la 2, kwa mfano 26+32?" Walimu walikadiria kuwa asilimia 78 ya wanafunzi wao wanaweza kujumlisha namba hizo.

Katika utafiti huo huo, wahojaji walifanya tathmini ya ujuzi wa wanafunzi wa darasa la 2 na 3. Matokeo yalionesha kuwa ni asilimia 27 tu ya wanafunzi wa darasa la 2 na 3 ndio waliweza kusoma hadithi hiyo na kujibu maswali ya uelewa; na asilimia 32% tu ya wanafunzi hawa waliweza hesabu rahisi ya kujumlisha ya kiwango cha Darasa la 2 (kwa upimaji, kiwango cha Darasa la 2 kilielezwa kuwa ni kujumlisha namba kati ya 1 na 20, bila kubeba: 5+1, 11+4, 5+15). Matokeo yanaoneshwa kwenye Kielelezo 5.

**Kielelezo cha 5: Matokeo ya wanafunzi na makadirio ya mwalimu (% ufaulu)**




**Chanzo:** Utafiti wa awali wa RISE, 2019.


Walimu wa shule za msingi hukadiria ujuzi wa wanafunzi wao kwa kiwango cha juu sana. Lakini idadi ya wanafunzi wanaopata ujuzi huu ni chini ya nusu ya makadirio ya walimu. Hali hii inaweza kutokana na sababu mbalimbali. Pengine walimu wanajua hali halisi ya wanafunzi wao lakini, wanapoulizwa na mhojaji/mgeni, wanatia chumvi ufaulu wa wanafunzi wao. Au walimu hawajui kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wao, ingawa ushahidi wa utafiti unaonesha kuwa walimu husimamia majaribio na mitihani ya wanafunzi kipindi chote cha mwaka wa masomo na kusahihisha kazi za masomo za kufanyia nyumbani *(homework)*. Halikadhalika, muundo na muda wa tathmini ni muhimu: Tathmini kama hiyo ya Twaweza iliyofanyika mwishoni mwa mwaka ilionesha kuwa asilimia 41 ya wanafunzi wa darasa la 2 wanaweza kusoma hadithi – Matokeo haya yako juu kidogo lakini bado yako chini ya makadirio yaliyofanywa na walimu ya asilimia70.

Uwezekano mkubwa zaidi ni kwamba kutolingana huku kwa makadirio ya walimu na uwezo halisi wanafunzi kunatokana na walimu kutamani mafanikio hayo makubwa na kujizuia kuonesha udhaifu kwa watu wa nje. Kwa vyovyote vile, matokeo haya yanahitaji tathmini huru zaidi za mara kwa mara za ujifunzaji katika madarasa ya chini ya shule za msingi. Ujuzi wa kusoma na kuhesabu ni matokeo muhimu sana yanayoamua maisha ya kitaaluma ya watoto shuleni. Uelewa wa pamoja na sahihi kuhusu viwango vya ujifunzaji wa wanafunzi ni hitaji muhimu ambalo litasaidia jitihada za pamoja za kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi wote.

## Hali ya Shule

### Jambo la 6: Mazingira ya Kufundishia katika madarasa ya chini ni changamoto

**Kielelezo cha 6: Idadi ya wanafunzi darasani**




**Chanzo:** Utafiti wa awali wa RISE, 2019


Kielelezo cha 6 kinaonesha wastani wa ukubwa wa madarasa ambayo walimu hufundisha. Ukubwa wa darasa hukokotolewa kwa kuangalia jumla ya wanafunzi walioandikishwa kwenye darasa husika na idadi ya mikondo ambamo wanafunzi wanafundishwa. Kuna tofauti ya wazi kati ya ukubwa wa madarasa. Madarasa ya mwanzo (Darasa la 1-4) yana wanafunzi wengi zaidi, tofauti na madarasa ya juu (Darasa la 5-7) yana wanafunzi wachache.

Matokeo mengine ya utafiti huo (hayamo kwenye jedwali) yanaonesha kuwa walimu wanataja ukubwa wa madarasa kama mojawapo ya changamoto kubwa wanazokabiliana nazo wakati wa kutekeleza mtaala mpya wa KKK kwa madarasa ya mwanzo.

### Jambo la 7: Usimamizi wa walimu usio sawa

Walimu waliulizwa ni mara ngapi mwalimu mkuu au msaidizi wake anaingia darasani kuangalia ufundishaji. Matokeo yanaonesha kuwa aina hii ya usimamizi haina usawa: asilimia 41 ya walimu wanasema hakijawahi kufanyika kitu kama hicho, wakati asilimia 36 wanasema huwa unafanyika angalau mara moja kwa mwezi.

**Kielelezo cha 7: Ni mara ngapi mmoja wa viongozi wa shule ameingia darasani kuangalia ufundishaji wako?**




**Chanzo:** Utafiti wa awali wa RISE, 2019

## Hitimisho

Matokeo tajwa kwenye muhtasari huu yanatoa hoja muhimu ya kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi na utendaji wa mwalimu. Masuala matatu yanayohusiana yamejitokeza.

Kwanza, wanafunzi wana shauku kubwa ya kujifunza na wengi wao wanataka kazi zinazohitaji angalau elimu ya baada ya kuhitimu sekondari. Hata hivyo, tathmini huru za kujifunza kwenye tafiti za RISE zinaonesha kuwa wanafunzi wengi hawapati stadi na ujuzi wa msingi wa kuandika, kuhesabu na kusoma hadithi katika miaka yao ya mwanzo shuleni.

Pili, kwa wastani walimu hawapendelei kufundisha madarasa ya mwanzo ya shule za msingi. Hata hivyo, mtaala unaeleza kuwa madarasa haya ni madarasa muhimu ambapo wanafunzi wanapaswa kumudu stadi za msingi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, walimu hawajui uwezo wa wanafunzi wao kumudu stadi hizi za msingi, wanafanya makadirio ya uwezo na maendeleo ya watoto yaliyo mbali sana na uhalisia.

Tatu, mazingira ya kufundishia katika madarasa ya mwanzo ni magumu kwa sababu ya wingi wa wanafunzi.

Kwa ujumla, kiwango cha motisha na utendaji kazi kwa walimu wa madarasa ya mwanzo kinahitaji kuboreshwa ili kulinda matokeo ya msingi ya kujifunza kwa wanafunzi. Kuboresha motisha ya walimu kwenye mfumo mzima wa shule ya msingi ni moja ya changamoto ngumu zaidi kwa serikali duniani kote. Ushahidi unaoongezeka unaonesha kuwa mifumo ya malipo kulingana na utendaji kazi ulioundwa vizuri unaweza kusaidia kushughulikia tatizo hili kwa ufanisi.